TIMER NATIONAL SERIES
MAJARIBIO YA MTIHANI {5}
DARASA LA TANO KISWAHILI

Toleo la: 0012015

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu cha maswali na karatasi ya kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINA LAKO **JINA LA SHULE YAKO** ***Muda: Saa 1 dakika 40***

Soma vifungu vifuatavyo ukijaza mapengo 1-15.

Mihadarati ni __1__ za kulevya __2__ zinadhuru afya. Zipo za __3__ mbalimbali. Dawa __4__ ni za __5__, za kunywa na hata za kudunga. Ninawashauri __6__ kuzitumia dawa __7__. Unapoanza au kuzoea kuzitumia dawa hatimaye __8__ uzoevu __9__ ni mgumu kuacha. Kamwe usijaribu kuzitumia dawa __10__.

	A	B	C	D
1.	madawa	dawa	vidawa	vijidawa
2.	ambayo	ambalo	ambazo	ambavyo
3.	aina	haina	hana	hina
4.	ingine	mengine	nyingine	zingine
5.	kufuta	kufutwa	kuata	kuvuta
6.	msijaribu	mjaribu	mtajaribu	mlijaribu
7.	hii	hizi	hio	hivi
8.	utapata	hutapata	tazipata	talipata
9.	ambalo	ambazo	ambayo	ambao
10.	hivi	vile	hizi	hiyo

Hapo __11__ palikuwa na mvulana __12__ aliyeitwa Bidii. Bidii __13__ katika familia maskini sana. Wazazi __14__ walimwangalia mwana __15__ kwa matumaini makubwa kwani yeye ndiye alikuwa kifungua mimba.

11.	zamani	samani	samahani	kizamani
12.	kimoja	mmoja	moja	mumoja
13.	alitoka	ilitoka	kilitoka	walitoka
14.	wao	lake	wake	chake
15.	wake	ao	lao	wao

Kutoka swali la 16-30, jibu kulingana na maagizo.

16. Andika kwa maneno:
Watalii 696.
A. Watalii mia sita tisini na sita.
B. Watalii mia tisa sitini na tisa.
C. Watalii mia tisa tisini na sita.
D. Watalii sitini na tisa na sita.

17. Jibu la alamsiki ni
A. binuru B. alamsiki
C. ya kuonana D. kwa heri

18. Nyumba ya ndege in kiota, je nyumba ya konokono ni _____.
A. kizimba B. ghala
C. kichuguu D. kombe

19. Andika kwa wingi:
Kitoto kile kinalia.
A. Watoto wale wanalia.
B. Vitoto vile vinalia.
C. Matoto yale yanalia.
D. Toto yule yanalia.

20. Umbo hili huitwa



A. mchinjo kati
B. mraba
C. msambamba
D. mstatili

21. Kanusha:
Mwalimu ametoka nyumbani.
A. Mwalimu hakutoka nyumbani.
B. Mwalimu hajatoka nyumbani.
C. Mwalimu hujatoka nyumbani.
D. Mwalimu ameingia nyumbani.

22. Mtu afanyaye kazi ya kutengeneza vitu vya mbao ni
A. hamali B. seremala
C. sonara D. mhunzi

23. Malipo atoayo mtu kusafiri huitwa
A. nauli B. karo
C. mahari D. kiingilio

24. Wingi wa tunda ni matunda. Je, majina haya huwa katika ngeli gani?
A. LI-YA B. A-WA
C. KI-VI D. U-ZI

25. Yupi kati ya hawa hula ndege wengine?
A. Kasuku B. Batamzinga
C. Kipanga D. Chiriku

26. Kipi ni chombo cha sebuleni?
A. Kochi B. Karai
C. Seredani D. Mbuzi

27. Andika kinyume. Mtoto ameamka.
A. Mtoto amevaa B. Mtoto ameanikiwa
C. Watoto wameamka D. Mtoto amelala

28. Msimu wa baridi kali huitwa
A. kipupwe B. vuli
C. kiangazi D. mchoo

29. Dada yake mama ni
A. mjomba B. wifi
C. halati D. shangazi

30. Kamilisha methali:
Mgema akisifiwa tembo
A. huvunjika guu B. hutoka msituni
C. hunywewa D. hulitia maji

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.

Baba alikuwa mgonjwa hospitalini. Ugonjwa wake ulikuwa umeendelea muda mrefu na tulianza kupata taabu ya chakula. Pesa ambazo baba alikuwa ametuachia kabla ya kulazwa hospitalini zilikuwa zimekwisha. Mama hakuwa na kazi isipokuwa vibarua vya hapa na pale.

Nyumbani tulikuwa watoto wanne; mimi na ndugu zangu wawili wakubwa na mdogo wangu. Tuliamua kumsaidia mama kutafuta pesa za chakula. Badala ya yeye kwenda peke yake, tulienda pamoja naye. Siku kama hiyo hatukuweza kwenda shuleni lakini mwalimu wetu alielewa shida zetu. Wiki moja tulienda vibaruani mara mbili. Pesa tulizozipata zilituwezesha chakula cha wiki moja. Baada ya miezi mitatu baba alianza kupata nafuu. Ilimchukua mwezi mwingine mmoja kutoka hospitalini. Tulifurahi sana kumwona akiwa mzima tena.

31. Kabla ya ugonjwa wa baba yao, familia yake
    A. ilipata shida ya chakula.
    B. ilipata shida ya kupata viatu.
    C. ilipata shida ya kukosa karo.
    D. haikupata shida yoyote.

32. Pesa alizoziacha baba kabla ya kulazwa hospitalini;
    A. ziliibiwa
    B. zilikamilika
    C. zilikuwa mbali
    D. zilikuwa benki

33. Kulingana na habari ni watu wangapi walienda vibaruani?
    A. Wawili
    B. Mmoja
    C. Watano
    D. Watatu

34. Mwandishi alikuwa mtoto wa
    A. tatu
    B. nne
    C. kwanza
    D. pili

35. Watoto walienda kazi mara ngapi kwa wiki?
    A. Tatu
    B. Nne
    C. Mbili
    D. Moja

36. Pesa zinazolipwa shuleni kwa malipo ya masomo huitwa
    A. ujira
    B. karo
    C. nauli
    D. mshahara

37. Kupata nafuu maana yake ni
    A. bei ya juu
    B. kupona
    C. kuugua sana
    D. kufa

38. Mwalimu wa shule
    A. hakuwa na huruma.
    B. alielewa kazi yake.
    C. alikuwa mkali.
    D. alielewa shida za watoto hao.

39. Baba alikaa hospitalini miezi
    A. mitatu
    B. miwili
    C. minne
    D. mmoja

40. Hospitali ndogo huitwa
    A. karakana
    B. maabara
    C. zahanati
    D. maktaba

Soma taarifa ifuatayo kisha jibu maswali 41-50.

Kuna michezo mingi sana kote ulimwenguni. Kuna michezo kama vile kandanda, riadha, netiboli na kadhalika.

Michezo ina faida kwetu sisi. Mbali na kuifanya miili yetu iwe na afya nzuri, mchezo humsaidia mtu kupitisha wakati wake vizuri badala ya kuingilia mambo yasiyofaa.

Si lazima mtu awe na kipawa maalum katika michezo. Mtu yeyote anaweza kushiriki katika michezo mbalimbali. Wakati mzuri wa kufanya michezo ni baada ya shule au baada ya kazi.

Michezo ina faida sana kwa mwanafunzi. Humsaidia kuwa na nidhamu maishani. Humfunza kuwa mtu hawezi kushinda kila wakati. Katika jamii, michezo huleta pamoja makabila mbalimbali hivyo basi kuchangia katika kuondoa ukabila.

41. Ni watu gani wanaoweza kushiriki katika michezo?
    A. Wanafunzi
    B. Wanaume
    C. Wanawake
    D. Watu wote

42. Wakati mzuri wa kufanya michezo ni
    A. wakati wowote.
    B. asubuhi.
    C. baada ya kazi.
    D. baada ya kula.

43. Michezo humsaidia mwanafunzi kuwa
    A. mkali
    B. mjinga
    C. mvivu
    D. na adabu

44. Michezo huwafunza wanafunzi kuwa
    A. lazima washinde.
    B. uvivu ni mzuri.
    C. ushindi haupatikani kila siku.
    D. wazee hawafai kucheza.

45. Jumla ya michezo mingapi iliyotajwa hapa?
    A. Saba
    B. Mitano
    C. Kumi
    D. Mitatu

46. Katika jamii michezo ina faida gani?
    A. Kuleta ukabila.
    B. Kumaliza ukabila.
    C. Kueneza chuki.
    D. Kuongeza uadui.

47. Ni sahihi kusema kuwa
    A. mchezo huleta chuki.
    B. michezo hujenga miili.
    C. michezo huzidisha ukabila.
    D. michezo imetengewa wanafunzi na wanaume.

48. Mchezo wa kandanda huchezwa na watu wangapi katika kila timu?
    A. Saba
    B. Kumi
    C. Kumi na wawili
    D. Kumi na mmoja

49. Wachezaji wengi pamoja huitwa
    A. kikosi
    B. kikoa
    C. timu
    D. kaumu ya watu

50. Kichwa mwafaka kwa taarifa hii ni
    A. Ukabila
    B. Mchezo wa kandanda
    C. Michezo
    D. Faida ya michezo